OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
SHULE YA SEKONDARI MBAGALA

Simu: +255 713 516786
+255 714624950

Email: mbagalasec@gmail.com

S. L. P 46357
DAR ES SALAAM
TANZANIA

Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi;
……
S.L.P ……...
…….

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MBAGALA. HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE, MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA 2022/2023.

1.0 Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika Shule hii mwaka 2022/2023 tahasusi ya ……..
Shule ya Sekondari Mbagala ipo umbali wa Kilometa 10.1, Kusini mwa Manispaa ya Temeke.

Muhula wa masomo kwa mwaka huu utaanza tarehe ....., hivyomwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni sikuya tarehe.....saa 2:00 asubuhi akiwapamoja na mzazi/mlezi.

Ili usajiliwe unapaswa kuja na Nakala ya cheti cha kuzaliwa pamoja na matokeo ya kidato cha nne (Notification of Results), vinginevyo hutosajiliwa.

1.1 SARE YA SHULE

(a) WASICHANA

i. Sketi (2) eggyplant/brownish purple **(Mshono Rinda Box).** Shati (2)nyeupe (tetron) mikono mifupi. Sample ya kitambaa inapatikana shuleni
ii. Nguo itakayovaliwa ndani ya shati iwe nyeupe mfano vest au singlet.
iii. Wanafunzi wanaovaa juba liwe jeupe refu kupita usawa wa nyonga. Shati mbili za mikono mirefu zenye vifungo mbele na sketi ndefu. Nembo ya shule ishonewe kwenye juba.

iv. Viatu vya ngozi vyeusi (jozi mbili) viwe vya kufunga na kamba na visiwe vinapiga kelele, viwe vinafunika kabisa (visiwe vya wazi) na visiwe na kisigino kirefu.
v. Soksi nyeupe ndefu(Stocking) sio za kuonyesha mwili.
vi. Sweta lifanane na rangi ya sketi.
vii. Hijabu itavaliwa na wasichana waislamu tu wanaopenda **(ya sketi ndefu na Nusu Kanzu).**
viii. T-shirt zinapatikana shuleni.
ix. Wasichana wanaruhusiwa kusuka nywele za mistari ya kurudi nyuma (twende kilioni) zisizopungua **5** na **7.**
x. Nembo ya Shule.
xi. Nguo za michezo ni track suit ya dark blue pamoja na raba nyeupe zisizo na urembo wowote.
xii. Tie inayofanana na rangi ya Sketi.

(b) SARE YA SHULE KWAWAVULANA

i. Suruali mbili (2) rangi eggyplant/brownish purple **(isipungue inchi "16" chini)**
ii. Shati nyeupe mbili (2) mikono mifupi tetroni.
iii. Nguo itakayovaliwa ndani ya shati iwe nyeupe mfano vest au singlet.
iv. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba (jozi2).
v. Soksi nyeusi (jozi 2).
vi. T- shirt zinapatikana shuleni.
vii. Mkanda mweusi wenye bakoli ya kawaida.
viii. Sweta lifanane na rangi ya suruali.
ix. Nembo ya shule.
x. Nguo za michezo ni track suit ya dark blue pamoja na raba nyeupe zisizo na urembo.
xi. Tie inayofanana na rangi ya suruali

MFANO WA UNIFORM KAMA ULIVYO KWENYE PICHA

1.2 ADA NA MICHANGO YASHULE

(a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 20,000.00/= Unaweza kulipia kiasi cha shilingi 10,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa maramoja.

(b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi/mlezi ni:-

Na.	AINA YA MCHANGO	KIASI CHA FEDHA (Tshs.)
1.	Taaluma	20,000.00
2.	Tahadhari	5,000.00
3.	Vibarua na walinzi	30,000.00
4.	Huduma ya kwanza	5,000.00
5.	Kitambulisho na Picha	6,000.00
6.	Mitihani ya Mock	20,000.00
7.	Matengenezo/Ukarabati	15,000.00
8.	Nembo	3,000.00
	JUMLA	**104,000/-**

Fedha zote za ada pamoja na michango zilipwe kupitia akaunti ya shule yenye Namba ***A/C*** **20703500450 NMB**. Jina la Akaunti ni **MBAGALA SECONDARY SCHOOL**. Baada ya malipo **BPS** ziwasilishwe shuleni.

2.0 VIFAA VIFUATAVYO VILETWE SHULENI.

(a) Ream 1 ya A4. Aina ya Monde au Rotatrim au NOPA.

(b) VIFAA VYA USAFI.

Na.	TAHASUSI	AINA YA KIFAA
1.	HKL & HGL	Hard Broom na Sabuni ya Maji Lita tano (5) aina ya **TARMOL**
2.	CBG	Mopper & Moping basin.
3.	EGM	Squeezer na sabuni ya maji lita 5 aina ya **TARMOL**.
4.	HGE	Fagio laini la ndani la kisasa (soft broom) pamoja na brash ndogo ya kusugulia masink ya chooni na panga
5.	HGK	Hard broom & Slasher na Jembe

2.1 VIFAA BINAFSI VYAMWANAFUNZI.

- Madaftari makubwa (counter book) **7** quire 4.
- Mathematical set na Scientific Calculator (HGE, EGM & CBG)
- Vitabu (watapewa majina ya vitabu hivyo na walimu wao wa masomo) Mf. Somo la Biolojia
  - ✓ Biological science 3rd edition 2011 by D.J Tayler N.P.O
  - ✓ Green and G.W. Staut
  - ✓ Guide to dissection by HGQ Rowett, M.A and M.I Biology
  - ✓ Dissection kit
- Four figure (mathematical table) – EGM, HGE& CBG
- Begi jeusi la mgongoni.
- Kamusi (Dictionary)
- Graph pads

  NB: Mzazi anashauriwa kumnunulia mwanafunzi walau nakala moja ya kitabu kwa masomo anayosoma Orodha ya majina ya vitabu vinavyohitajika inapatikana shuleni

2.2 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu **Na. 25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **Na. 10** ya mwaka **1995.** Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya Elimu chini ya **Ofisi ya Rais (TAMISEMI)** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu**.**

3.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujuma.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, Kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele kwa mitindo isiyokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi

wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi unaokubalika na uongozi wa shule.

vii. Kufuga ndevu.
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
xi. Kupata ujauzito au kutoaujauzito.
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimbamsichana.
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xvi. Kudharau bendera ya Taifa.
xvii. Kufanya jaribio la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xviii. Uharibifu wa mali ya Umma kwamakusudi.

3.1 VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU VIRUDISHWE SHULENI BAADA YA KUJAZWA KIKAMILIFU.

a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (**Medical Examination Form**) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.
b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa yajinai.
c) Fomu ya wazazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

3.2 MENGINEYO:

Matumizi na mahitaji ya mwanafunzi yanategemea zaidi Mzazi/Mlezi. Ni imani yetu kuwa utampa mwanao msaada wa kila aina ili aweze kusoma kwa makini na kwa ufanisi.

NB: Mwanafunzi asipokuja na mahitaji hayo hatapokelewa.
Tafadhali soma kwa makini maelekezo haya kwa utekelezaji fanisi. Shule haipo tayari kwa usumbufu wowote unaohusiana na mahitaji haya muhimu.

MWISHO

Uongozi wa Shule unakutakia maandalizi mema ya kujiunga na shule yetu.
Ni Matumaini yetu utazingatia kanuni na sheria za shule ili lengo lililokuleta shuleni kukamilika.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

…….
MARIAM A MUSHI

MKUU WA SHULE.

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA AHADI

Mkuu wa Shule,

Mbagala Shule ya Sekondari

S.L.P 46357,

DAR ES SALAAM

Kwa mwanafunzi.

Mimi .....ninakubali nafasi niliyopewa kuingia Kidatocha…… mwaka.....Katika shule ya Mbagala Sekondari.

Naahidi kwamba:

1. Nitatii sheria zote za shule kama nilivyozisoma
2. Nitafanya bidii katika masomo na shughuli zote za shule.
3. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu, mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wowote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya shule ya Mbagala Sekondari.

MUNGU NISAIDIE:

Sahihi ya mwanafunzi……..
Tarehe……

KWA MZAZI/MLEZI:

Mimi (Jina Mzazi/Mlezi……
……

Mzazi/Mlezi wa……

Naahidi kwamba:

1. Nitampatia mwanangu mahitaji ya shule kama yalivyotajwa katika maelekezo ya kujiunga na shule
2. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakaohitajika (maoni, adhabu) katika kumlea mwanangu
3. Nitamhimiza mwanangu kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani (homework) na kufuatilia maendeleo yake na tabia yake shuleni.
4. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake.
5. Nitashirikiana na walimu kumweleza mwanangu maana ya shule na umuhimu wa kuwepo shuleni.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi…….. Tarehe……

FOMU YA USAJILI (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI)

A: IJAZWE NA MWANAFUNZI:

1. Jina kamili la mwanafunzi……....
2. Taifa……
3. Uraia…….. Picha ya mwanafunzi
4. Dini……..
5. Tarehe ya kuzaliwa……
6. Mahali alipozaliwa…… Wilaya……
7. Shule ya sekondari aliyosoma…….....
8. Tarehe ya kutoka shule aliyosoma……..
9. Nakala ya cheti chakuzaliwa
10. Cheti cha kumaliza kidato cha nne (Leaving certificate)
11. Nakala ya matokeo (Result slip kidato cha nne)

PICHA

B: MAELEZO BINAFSI YA MZAZI /MLEZI:

1. Jina kamili……..
2. Anuani kamili mjini Dar es salaam……
3. Sehemu unayoishi ..... Picha ya Mzazi/Mlezi
4. Mtaa……..
5. Namba ya nyumba…….
6. Simu ya mkononi:Baba……, Mama.....,
   Mlezi……..

PICHA

C: MAELEZO YA KIKAZI YA MZAZI/ MLEZI:

1. Jina la mwajiri na Idara…….
2. Anuani yake…… Simu namba……..…….
3. Kazi ya mzazi/ Mlezi (Meneja, Daktari, Mfanyabiashara n.k)……..

D: SOMO LA DINI

Mimi .....ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi..... Kidato cha ..... Ninaruhusu mtoto wangu kuhudhuria somo ladini ya .....Dhehebu la …….....Siku ya Jumatano akiwa shuleni Mbagala sekondari.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi……

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIAMBAGALA SECONDARY SCHOOL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To be filled by Government Medical officer and return to theHEAD OF SCHOOL Mbagala secondary school P.O. Box 46357,

A: **RE:** .....

Please examine above mentioned student and comment on his/her fitness by responding to the problems below. Say Yes or No if student has health problem and if yes then STATE.

Head mistress

Insert √ in the boxes provided

i.	Hearing	Yes ☐	No ☐
ii.	Speech	Yes ☐	No ☐
iii.	Sight	Yes ☐	No ☐
iv.	Ts	Yes ☐	No ☐
v.	B.P	Yes ☐	No ☐
vi.	Diabetes	Yes ☐	No ☐
vii.	Mental Case	Yes ☐	No ☐
viii.	Physical Disability	Yes ☐	No ☐

ix. Any other.....

.....

.....

.....

B: Recommend if the student is fit for studentship;

.....

.....

C: Any other advice.....

.....

Name.....

Signature.....

Date.....